# JARIDA LA KILIMO HIFADHI

**MACHI, 2020 • UKUBWA 6 • TOLEO 1**

| NDANI YA TOLEO HILI | Mfumo wa mbegu katika utekelezaji wa usalama wa chakula | Wasifu wa mshiriki: Help Channel Burundi | Kumtambulisha Lilian Zheke, ALTA wa Kusini mwa Afrika | ALTA Ratiba za Safari |
|---|---|---|---|---|

## Mfumo wa mbegu katika utekelezaji wa usalama wa chakula

***Na Jean Twilingiyumukiza, Mshauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha, Afrika ya kati na magharibi***

Uzalishaji na ugawaji wa mbegu bora zinaweza kuongeza mazao, lishe na ustahimilivu baina ya wakulima wadogo wadogo. Hata hivyo, shirika la chakula ulimwenguni FAO (FAO, no date) lilisema kuwa usalama wa chakula kwa jamii ya wakulima inategemea usalama wa mbegu zake.

Katika nchi nyingi mifumo miwili ya mbegu zinatawala. Sekta ya mbegu ilio rasmi inaendeshwa na mawakala wa serikali na shughuli za kibiashara ambazo zina toa mbegu zilizothibitishwa zenye utofauti na vyeti thabiti mbali mbali. (Louwaars & de Boef, 2012). Kusini mwa jangwa la Sahara (SSA), Benki ya dunia (WB) inakadiria asilimia 5-10 tu ya wakulima wananunua mbegu kutoka kwenye sekta zilizo rasmi. Sekta ya mbegu zisizo rasmi inahusisha mbegu zilizohifadhiwa na mkulima binafsi au zimechukuliwa kutoka kwa majirani au sokoni. Mbegu kutoka sekta hizi ni rahisi kupatikana na ni nafuu, lakini ni za ubora hafifu (ACBIO, 2015). Sekta zisizo rasmi zinaweza kutoa mbegu zenye usajili mbali mbali lakini pia michanganyiko ya kiasili. Inatoa kati ya asilimia 80 -90 ya mbegu zinazopandwa na wakulima ulimwenguni. (Practice Brief 6).



**Mazao funika, kama Kanavalia yamepandwa chini ya mahindi yameenea kwa takriban muda wa miaka kuma, moja kati ya usambazaji wa mbegu na Miadi inayosaidiwa na CFGB.**

### MANENO MAKUU YANAYOTUMIKA KATIKA MIFUMO YA MBEGU

- **Mazao ya mchavusho pweke / mchavusho tambuko:** mazao mengi, ikiwa ni pamoja na maharage, mchele, ngano na nyanya;

Canadian Foodgrains Bank
A Christian Response to Hunger

**Maafisa ufundi wa kilimo hifadhi wa CFGB**

**Jean Twilingiyumukiza**
jean.twilingiyumukiza@tearfund.org

**Neil Rowe Miller**
neil.rowe-miller@tearfund.org

**Lilian Zheke**
lilian.zheke@tearfund.org

zinaweza kutoa mbegu bila kupokea chavuo na hivyo yanazalisha “mbegu halisi” kupitia vizazi hadi vizazi. Mazao ya mchavusho tambuko, kama vile mahindi na alizeti, zinazaa kwa kuchavushwa na mimea kupitia upepo na wadudu. Isipokuwa zinapandwa kwa kutenganishwa (aidha hakika au kupanda kwa nyakati tofauti tofauti) hazitozaa halisia kuanzia kizazi hadi kizazi. Mimea mingine; kama mtikiti, boga, pamba na mbaazi; zinazalishwa kwa mchavusho pweke na tambuko. Tabia zake zinaweza kuamua ni kwa kiasi gani zinahitaji kutengwa ili kutoa mbegu safi.

- **Aina za mbegu za mtindo huru (OPVs)** ni zile ambazo zina toa mbegu ambazo zina vinasaba vinavyofanana na mmea ambao ni mzazi. Kama zao litachavushwa kwa mchavusho tambuko, aina ya mbegu zinazozalishwa kwa mtindo huru zitahitaji kutengwa ili kutoa mbegu halisi. (FAO, 2010).

- **Mbegu chotara** zinazalishwa kwa mchavusho tambuko kupitia vizazi tofauti kwa ajili ya uzalishaji. Mbegu chotara kwa ujumla zinatoa mimea yenye nguvu na mfanano mkubwa. Kama mbegu chotara ikirudiwa kupandwa kwa vizazi viwili, mazalio yanakua sio nakala halisi ya wazazi, hivyo wakulima lazima wanunue mbegu mpya kila msimu. Mahindi ndio yanatumika sana kama mbegu chotara.

- **Mbegu zilizothibitishwa** zinachunguzwa na kupimwa na mawakala wa serikali kwa ajili ya usafi wa vinasaba, majaribio ya mbegu na kuwa huru na magonjwa na magugu. Aina tu zilizosajiliwa na mawakala wa serikali ndizo zinazothibitishwa (FAO, 2018).

- **Mbegu zilizodhibitishwa ubora (QDS)** zinazalishwa na kuuzwa na wakulima na mashirika ya kijani ambao sio wauzaji wa mbegu waliosajiliwa. Aina zote za kisasa na za kienyeji zinajumuishwa. Mamlaka za kiserikali zinatambulisha aina zipi ni sahili/ muafaka na zinachunguza angalau asilimia 10 ya mashamba ya mbegu zinazotangazwa ubora (FAO, 2018)

**Mbinu za kuzalisha mbegu za kijamii** zinaweza kusaidia wakulima kupata mbegu bora,na rahisi kupatikana kwenye mazingira ambayo sekta iliyo rasmi haitendi au ni batilifu. Ili iwe endelevu, mipango kama hii inatakiwa kuendeshwa kama biashara ya kujipatia faida, kuanza na upimaji wa masoko kwa kina. Ili kupunguza uwezo mkubwa wa mazao kuharibika, maeneo ya uzalishaji yatatakiwa kuwa karibu na maeneo ya umwagiliaji au maeneo yenye mvua za mfululizo. Uzalishaji wa vikundi na kwa wingi wa mbegu kutoka kwa wakulima wengi hua ni changamoto kwa sababu ya ufatiliaji hafifu na ubora usiolingana. Wakulima huwa wanatunza mbegu zao bora kwa ajili ya matumizi yao na ni ngumu kufatilia vinasaba safi ya mbegu nyingi kutoka kwa wakulima wengi.

Njia mbadala wa kukusanya ni kusaidia wakulima binafsi kupanda na kuuza mbegu zilizozibitishwa ubora( QDS). Udhibiti wa ubora ni rahisi kwa kua wazalishaji baadhi wanahusishwa na masoko ya mbegu zinazotangazwa ubora ni pana kwa kua inaweza kuuzwa kwenye masoko ya kijamii na kutangazwa nje ya jamii. Walakini mbinu za uzalishaji, changamoto ya kutangaza mbegu za aina ya mtindo huru ( OPVs) itaendelea kwa kuwa wakulima hupendelea kutunza na kurudia rudia kupanda mbegu kuliko kulipia gharama kubwa kwa ajili ya mbegu zilizothibitishwa na zilizozibitishwa ubora( QDS).

Mojawapo ya mifano ya mbinu ambazo zinafanya kazi ya kutoa mbegu na ilitekelezwa na ofisi ya maendeleo ya kanisa ya kievanjelisti (ODE), mshiriki mwenza wa MCC/ CFGB kule Burkina Faso. ODE waliwafunza wakulima binafsi ishirini katika uzalishaji wa mbegu, kuweka mfumo wa kuanzia, na kuwaunganisha kwenye shughuli za mbegu kitaifa kwa ajili ya uchunguzi na uthibitisho. Mwaka 2017, wakulima wanatoa tani 34.7 ya mahindi yaliyozibitishwa ubora, mtama, kunde na mchele.

**Mbinu za kutunza mbegu za kijamii** zinaweza kuwasaidia wakulima kutunza vinasaba mbali mbali na mazao ya kibiashara, huku tunazuia ushawishi wa kutumia kama chakula kipindi cha njaa. Hifadhi za mbegu ambazo wakulima hukusanya na kutunza mbegu kwa pamoja, ilizoeleka sana kwenye miradi iliyosaidiwa na CFGB, lakini walihangaika na masuala ya usimamizi na udhibiti wa ubora na mara nyingi zinaisha pale ambapo rasilimali za mradi zimekatishwa. Ili kutekeleza masuala ya udhibiti wa ubora, vikundi vya wakulima wanaungwa mkono na jumuiya ya waevanjelisti wa Sierra Leone, mshiriki wa Tearfund Canada/CFGB, wanatunza mbegu kwenye hifadhi moja, lakini wanatunza mbegu za kila mkulima kwenye chombo chake mwenyewe.



Kikundi cha *Tabacsne* (uvumilivu wa sisi kwa sisi) kilichopo kijiji cha Bross kule , Sierra Leone, hifadhi ya mbegu za karanga kwa mtu binafsi ili kuzuia ushawishi wa kutumia mbegu kwa ajili ya chakula .

Uhifadhi wa mbegu katika nyumba moja moja ni rahisi kusimamia na kuwafundisha wakulima kuhusu njia bora za uhifadhi (kama vile begi la hermetic) imekua ni njia thabiti na ya muda mrefu, ingawa vishawishi vya kutumia mbegu zilizohifadhiwa manyumbani mara nyingi ni tatizo. Wakulima wanaofanya kazi na dayosisi ya Tanganyika ya kati, washiriki wa Tearfund Canada/ CFGB walitatua ushawishi huu kwa kutunza mahindi kwenye plastic, chini ya ardhi, mashimo yaliyofunikwa ambazo zinafunikwa mpaka zitakapohitajika.

***Kusambaza mbegu:*** mashirika yasio ya kiserikali na miradi ya kiserikali mara nyingi huhusisha usambazaji wa mbegu kama sehemu ya usalama wa chakula. Moja ya sababu ya hizi shughuli ni kuanzisha aina mpya, kwa mfano mazao ya mbolea ya kijani na mafunika ardhi .Ambazo matumizi yake kwenye miradi ya SSA inayotegemea CFGB imeongezeka kutoka kiganja cha mkono mpaka wakulima 20,000 leo walisaidiwa na usambazaji wa mbegu.

Sababu ya pili ya kusambaza mbegu ni miradi ya usalama wa chakula ili kuboresha vinasaba vya mazao yanayoendelea kuwepo. Ingawaje, “si aina zote za kisasa zinazotolewa na sekta zisizo rasmi zimeboreshwa” Zaidi ya zile ambazo wakulima wanaendelea kupanda. Kwa sababu hii, wakati wa kutambulisha aina mpya wakulima wanatakiwa wapatiwe mbegu za kutosha kujaribia kwenye sehemu ndogo karibu na eneo la uangalizi na aina ya mbegu ambayo mkulima ameizoea. Majibu ya huu mlinganisho yanatakiwa kukusanywa na kupimwa kabla ya kuanza kudumisha hii aina mpya sehemu zingine.

Sababu ya tatu ambayo huwa inatajwa katika usambazaji mbegu ni kuanzisha uhamasishaji wa wakulima kushiriki katika mradi. Uzoefu unaonyesha kuwa utekelezaji huu utawachanganya wakulima na kuweka wazo bandia kuwa wanatamani mafunzo na kazi zingine, ili hali maazimio yao ni mbegu za bure. Miradi ambayo inatumia mfumo huu inatakiwa kufanya hivyo katika kipindi cha mwanzo cha ushiriki wa wakulima, na wanatakiwa kuweka wazi kuwa wakulima watatakiwa kutunza mbegu kwa misimu ya baadae.

Miradi ambayo inamtaka mkulima kurudisha mbegu alizopewa inakumbana na chagamoto za ziada. Kusimamia usafi wa vinasaba na ubora wa mbegu ni ngumu, na utaratibu wa kukusanya , kuandaa, kutunza na kufanya usambazaji wa mbegu inaleta mzigo mkubwa kwa shirika. Miradi mingi ni bora inunue mbegu mpya, mbegu za biashara kila mwaka, na kuwahamasisha wakulima wagawane mbegu na majirani zao kuliko kujisumbua kufatilia mapatano yao.

Mwisho kabisa, miradi inatakiwa ifanye kazi pamoja na kuliko kufanya upinzani dhidi ya wafanyabiashara wadogo. Pale ambapo shirika binafsi au serikali inaingiza kiasi kikubwa cha mbegu kwenye jamii wanaua biashara za wauza mbegu wakujitegemea. Wauza mbegu hao hao wanaweza kutumika katika upatikanaji wa mbegu, hivyo kupunguza kazi kwa wafanyakazi wa mashirika binafsi. Mfumo wa Ankara pia unawasaidia wafanyabiashara wadogo na kuwapa wakulima machaguo mengi juu ya aina ya mbegu wachukue na kwa nani.

## Wasifu wa mshiriki: Help Channel Burundi

***Na Jean Twilingiyumukiza, Mshauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha, Afrika ya kati na magharibi***

Help Channel Burundi (HCB) ilianzishwa mwaka 2000 na kusajiliwa kama shirika lisilo la kiserikalii mwaka 2003. Kauli yake ya mwanzo ilikuwa ni kuitikia wito wa migogoro ya kibinadamu ilioipata Burundi iliyotokea baada ya  na vita ya mwaka 1990. Shirika sasa linaendelea kufanya kazi katika usalama wa chakula, haki za binadamu, ulinzi wa watoto, pamoja na usalama wa mazingira.

HCB imefanya kazi kupunguza ukosefu wa usalama wa chakula katika majimbo ya Kirundo, Rutana na Makamba kwa miaka kumi. Mikakati ya mwanzo inahusisha chakula cha misaada ya moja kwa moja, upandaji wa miti, makinga maji kwa ajii ya mmomonyoko wa ardhi na kukarabati barabara za vijijini katika maandalizi ya chakula kwa ajili ya kazi. Kufuatana na uchambuzi wa hali iliyofanyika mwaka 2016, Help Channel ilianza utafiti wa mikakati ambayo itafanya uzalishaji na usalama wa chakula kwa muda mrefu. Hii ilipelekea mradi wa *Ikigega Iwacu (*ilizalisha ghala la matunzo manyumbani) iliyoanza na kwa msaada wa MCC/CFGB mwaka 2016. Mradi umefundisha zaidi ya nyumba 1267 katika jamii sita, pamoja na tatu zile ambazo walifanya kazi miaka ya nyuma na watatu wapya. Sehemu za miradi iliohusisha uzalishaji wa kilimo kwa kukuza kilimo hifadhi (KH) na njia nyingine nzuri za kilimo, na shughuli baada ya kuvuna, pamoja na teknolojia ya utunzaji.



**Kamikazi Jeanette (l), mtaalamu wa kilimo HCB, atembelea shamba la kilimo hifadhi jamii ya Gahe**

Kilimo kinabaki kuwa sekta kuu Burundi na Zaidi ya asilimia 90% ya watu inategemea kilimo kwa ajili ya maisha yao. Mazao makuu ya chakula ni mahindi, mchele, mihogo, kiazi kitamu na ndizi ya chakula.kuna misimu mitatu ya kupanda. Msimu A (mvua nyingi) kuanzia katikati ya Septemba na Februari, ambapo wakulima wengi hupanda mahindi. Msimu B (mvua chache) unaanza katikati ya Februari na mwishoni mwa Mei na wakulima wanalenga uzalishaji wa maharage. Msimu C (msimu wa kiangazi).

Licha ya hizi changamoto, katika jamii sita ambapo mradi wa Ikigenga Iwaku unatekelezwa, usalama wa chakula sana. Wastani wa chakula kwa siku ambao washiriki wameripoti kuwa wanakula ilienda kutoka 1.7 tangu muda wa uchunguzi wa awali mpaka 2.5 mwaka 2019. Alama zinazoonyesha ulaji tofauti tofauti wa wanawake ilipanda kutoka 2.5 mpaka 4.4, ilhali ugawaji wa chakula cha kutosha manyumbani kwa mwezi ilitoka kuanzia miezi 6.6  mpaka 9.5 .tathmini za hivi karibuni zinaonyesha kuwa ubora wa vyakula na uthabiti wa upatikanaji wa chakula kuboreshwa.

HCB imependekeza mradi wa miaka mitano kwa MCC/CFGB ili kutengeneza mafanikio, na kuendelea kushughulikia suala la wasiwasi wa usalama wa chakula  kule Burundi, kwa kujipanua katika jamii mpya ilhali tunaendelea na jamii tulizokua. Lengo jipya la pendekezo ni kuajiri vikundi 144 vya kijamii  (nyumba 3,840) kwa kukuza kilimo hifadhi na masomo mengine

yanayoendania ili kuongeza uzalishaji wa kilimo, vipato vya familia, usawa wa kijinsia na usalama wa chakula

## Kumtambulisha Lilian Zheke, ALTA wa Kusini mwa Afrika

Tunafuraha kumkaribisha Lilian Zheke kama Afisa Ushauri wa kifundi wa kilimo na maisha wetu mpya. Lilian ataungana na Neil Rowe Miller, alieko Tanzania na Jean Twilingiyumukiza, alieko Rwanda, ili kujaza nafasi kwenye timu ya wataalamu wa kiufundi wa Canadian food Grains Bank na Tearfund UK katika miradi ya kilimo na ufugaji kusini mwa jangwa la Sahara.



**Lilian Zheke akiendesha somo la kuhusu masoko yaliyofanyika katika warsha Malawi nchini kote.**

Lilian amejikita Harare, Zimbabwe katika ofisi za Tearfund, na akaanza kufanya kazi Januari, 2020. Nchi za kipaumbele kwake ni pamoja na Zimbabwe na Malawi, ingawa atasaidia utekelezaji kule Zambia, Msumbiji na Uganda.

Lilian ana uzoefu wa kufanya kazi katika serikali na sekta binafsi. Zaidi ya hayo mafunzo ya msingi ya kilimo, analeta ujuzi thabiti katika utafiti wa masoko ya kilimo, hali ya hewa, and baadhi ya ujuzi katika ukuzaji wa mifugo. Anafanya mazoezi ya kimethodisti na tumebarikiwa kuwa nae kwenye timu yetu.

## ALTA Ratiba za Safari

### *Jean Twilingiyumukiza*

**9-13 Machi 2020**
***Freetown na Port Loko, Sierra Leone***
Kutembelea mradi: AEL (Liberia) na EFSL (Sierra Leone)

**18 -20 Machi, 2020**
***Gicumbi & Bugesera Rwanda***
Kutembelea RICA na maeneo ya utafiti

**28 – 30 April, 2020**
***Goma, DRC***
Kikao na karakana ya nchini nzima

**26 -29 Mei, 2020**
***Bukavu, DRC***
Kutembelea mradi wa CBM/CBCA Muku

### *Neil Rowe Miller*

**9 -13 Machi, 2020**
***Freetown na Port Loko, Sierra Leone***
Ziara ya mradi: AEL (Liberia) na EFSL (Sierra Leone)

**6 – 10 Aprili, 2020**
***Kitui, Kenya***
Warsha ya Kenya-wide patner

**10 – 17 May, 2020**
***Nebbi &Bidibidi, Uganda***
Project visits
Ziara za miradi

### *Lilian Zheke*

**30 Machi -2 Aprili 2020**
***Mutare, Zimbabwe***
Ziara ya kufahamiana kwa EFZ

**6 -7 Aprili, 2020**
***Bulawayo, Zimbabwe***
Ziara ya kufahamiana kwa BICC

**19 Aprili – 2 Mei 2020**
***Teddington, UK***
Tearfund Orientation

**11 -16 Mei 2020**
***Malawi***
Safari ya kufahamiana kwa Ag CARE pamoja na CARD

**25 – 30 Mei, 2020**
***Harare, Zimbabwe***
EFZ/ Mafunzo ya shughuli baada ya mavuno